JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714 - 2175 | Toleo Na: 009 | Januari - Machi, 2022

WAKULIMA WA KAHAWA KAGERA KUNUFAIKA, SERIKALI YAONDOA TOZO 42 – WAZIRI MKUU

BENKI YA TAIFA YA USHIRIKA KUANZISHWA

"Ushirika – Pamoja Tujenge Uchumi"

YALIYOMO

KUTOKA KWA MRAJIS	03
WAKULIMA WA KAHAWA KAGERA KUNUFAIKA, TOZO 42 ZAONDOLEWA	04
BENKI YA TAIFA YA USHIRIKA KUANZISHWA	05
SITAKI KUSIKIA MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA	06
UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAFUNZO KWA VYAMA VYA USHIRIKA KUIMARISHWA	07
TCDC NA TANTRADE ZASAINI MAKUBALIANO	09
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YATEMBELEA SHAMBA LA USHIRIKA WA ZABIBU CHABUMA – AMCOS	10
USAJILI, UTOAJI LESENI NA USIMAMIZI	11
SACCOS YAIUNGA MKONO SERIKALI UJENZI WA MADARASA MKOANI MBEYA	12
MIONGOZO KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA	13
KIKAO KAZI NA MAFUNZO KWA WATEKELEZAJI WA SHERIA YA USHIRIKA	15
TCDC YATOA MSAADA KWA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUMU WA KIJII CHA MATUMANI DODOMA	16
MIKAKATI KUONDOA HATI MBAYA NA ZISIZORIDHISHA KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA VYA KOROSHO NA TUMBAKU	17
SACCOS ZATAKIWA KUANDAA NA KUWASILISHA TAARIFA ZA UTENDAJI	19
WANAWAKE WALIOPO KATIKA SACCOS KANDA YA KASKAZINI WATOA VIFAA KINGA, HOSPITALI YA MAWENZI	20
BENKI YA USHIRIKA KILIMANJARO YAADHIMISHA MWAKA MMOJA KWA MAFANIKIO	21
VIONGOZI BODI YA TFC WALA KIAPO CHA MAADILI	22
UJUMBE WA TANZANIA WAFANYA ZIARA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA UGANDA	22
TANZANIA KUSHIRIKIANA NA BURUNDI KATIKA SEKTA YA USHIRIKA	23
TUME YA USHIRIKA NA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI ZA ANDAA MPANGO KAZI WA KUIMARISHA USHIRIKA KATIKA SEKTA YA MIFUGO	24
TCDC SACCOS YAANZISHA UWAKALA WA HUDUMA ZA KIFEDHA	25
WAJUMBE WA BODI NJORECU WAPATIWA MAFUNZO YA UONGOZI NA UTAWALA BORA	26
MAFANIKIO YA USHIRIKA SHINYANGA – AMCOS YANUNUA TREKTA	27

KUTOKA KWA MRAJIS

Ndugu Wasomaji,
Niwakaribishe tena katika Jarida la Ushirika, Toleo la Tisa, ambalo ni mfululizo wa majarida yanayoandaliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania katika jitihada za kuelimisha na kuhamasisha masuala na hatua mbalimbali zinazofanyika katika Sekta ya Ushirika.

Benki ya Ushirika Itawawezesha Wanaushirika Kumiliki Uchumi wao

Kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika kutawawezesha Wanaushirika na Wanaanchi kwa ujumla kumiliki Uchumi wao na kupata huduma kwa urahisi, hii itawasaidia kupata mitaji itakayotolewa kwa riba ndogo ukilinganisha na Taasisi nyingine za kifedha. Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, imechukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuhakisha kuwa Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) inaendelea kuwepo na kuwezesha kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika.

Dkt. Benson Ndiege, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).

Hatua zilizochukuliwa na Tume ni pamoja na kuhamasisha SACCOS zote zilizokuwa zimewekeza kwenye Benki ya KCBL kukubali kufanya mabadiliko na kuruhusu akiba zilizokuwa zimewekezwa ziwe sehemu ya hisa za Benki kwa lengo la kuongeza mtaji wa Benki. Pia, kuhamasisha wanaushirika kuwekeza kwenye Benki pamoja na kutoa maelekezo kwa TFC kuhamisha Fedha zilizokuwa zimekusanywa zenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni mia nne kuingizwa KCBL kwa lengo la kuiongozea uwezo wa kifedha na kupata Mtaji unaotakiwa.

Aidha, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imeendelea kufanya Usimamizi na kutoa maelekezo kwa KCBL ikiwemo kufanya tathmini ya Bajeti ya KCBL, kutoa ushauri na kuidhinisha bajeti hiyo ili kuendana na mahitaji ya soko la fedha.

WAKULIMA WA KAHAWA KAGERA KUNUFAIKA, TOZO 42 ZAONDOLEWA

Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, ametangaza uamuzi wa Serikali wa kuondoa tozo 42 kati ya 47 ambazo Wakulima wa Kahawa wa Mkoa wa Kagera walikuwa wanatozwa na kubaki tozo 5 ambazo zitakuwa na jumla ya Shilingi 267 kwa kila kilo ya Kahawa, kutoka Shilingi 830 za awali. Waziri Mkuu ametoa maamuzi hayo kufuatia Tume maalum aliyoiunda ili kupitia utaratibu na Mfumo wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika wa zao la Kahawa Mkoani Kagera.

Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, akizungumza kwenye Kikao Maalum cha Wadau wa zao la Kahawa mkoani Kagera.

Mheshimiwa Majaliwa amewaagiza viongozi wa vyama vya Ushirika, wasimamie vyama vyao kwa uaminifu na weledi ili kuwaletea tija Wakulima wanaouza mazao yao kupitia Vyama vyao vya Ushirika.

Waziri Mkuu ametoa maelekezo hayo Machi 29, 2022 kwenye Kikao Maalum cha Wadau wa zao la Kahawa mkoani Kagera kilichofanyika Wilayani Karagwe Mkoani Kagera.

"Tozo hizi zimekuwa nyingi mno na si tija kwa Mkulima ambaye sisi tunapaswa kumsimamia na kulisimamia zao hili kuepusha kutoroshwa na kuuzwa nchi za jirani," alisema Mhe. Majaliwa.

Tozo zitakazobaki ni Uendelezaji wa zao la Kahawa (Shilingi 100), AMCOS (Shilingi 70), Union (Shilingi 30), Halmashauri pamoja na vifungashio.

Vilevile, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kuanzia sasa mauzo ya Kahawa katika Mkoa wa Kagera yatafanyika kwa njia ya mnada ambapo minada hiyo itafanyika kwenye ngazi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS).

Wanaushirika na Wadau wa Sekta ya Kahawa wakiwa kwenye Kikao Maalum cha Wadau wa zao la Kahawa mkoani Kagera kilichoongozwa na Waziri Mkuu.

BENKI YA TAIFA YA USHIRIKA KUANZISHWA

Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, amevitaka Vyama vya Ushirika kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika Tanzania (National Cooperative Bank - NCB) itakayomilikiwa na Wanaushirika wenyewe.

Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, akizungumza na Wanaushirika

Mheshimiwa Bashe alikuwa akizungumza na Viongozi wa Vyama vya Ushirika, Machi 17, 2022 Jijini Dodoma ambapo amesema Benki hiyo itaanza na kianzio cha Shilingi Bilioni 15 na hadi sasa kuna Shilingi Bilioni 3.3, ambapo Shilingi 443,997,550 zimekabidhiwa kwa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (KCBL) kutoka Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) zilizochangwa na baadhi ya Vyama vya Ushirika nchini.

Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, akikabidhi Hundi ya Shilingi 443,997,550 kwa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (KCBL) kutoka Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) zilizochangwa na baadhi ya Vyama vya Ushirika nchini.

Waziri wa Kilimo amesema kuwa Benki ya Ushirika ya Taifa itakuwa na Makao yake Makuu Jijini Dodoma na itakuwa na Matawi nchi nzima ambapo itavihudumia Vyama Vyote vya Ushirika vitakavyochangia mtaji wa kuanzisha Benki hiyo.

Aidha, Waziri Bashe amevitaka Vyama Vikuu vinavyosimamia Mazao Makuu ya kibiashara ya Pamba, Korosho, Kahawa na Tumbaku kusimamia ukusanyaji wa makato ya Wakulima yatakayowezesha kukuza Mtaji wa Benki hiyo kwa haraka; na amesema kila Mkulima atakayechangia atapewa Cheti cha umiliki wa Hisa za Benki hiyo.

Baadhi ya Wanaushirika waliohudhuria Mkutano ulioongozwa na Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, kuhusu kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika ya Taifa.

Kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika kutaviwezesha Vyama vya Ushirika kufanya biashara, kupata Mikopo yenye Riba nafuu na kuviwezesha kujiendesha kibiashara na kuwalinda Wanaushirika wakiwemo Wakulima, kutokunyonywa na Taasisi za Fedha zinazotoa Mikopo yenye Riba kubwa.

SITAKI KUSIKIA MIGOGORO KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA – MRAJIS

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amewataka Warajisi Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa kuhakikisha kuwa katika maeneo yao kunakuwa na udhibiti wa migogoro katika Vyama vya Ushirika.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, akizungumza na Warajisi Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa.

"Msisubiri migogoro iwe mikubwa katika Vyama, kwa kuwa inaharibu taswira ya Sekta ya Ushirika, hakikisheni mnashughulikia migogoro hiyo inapojitokeza na kutoa suluhisho; migogoro mingi inayofikishwa ngazi ya Taifa inaonyesha udhaifu wa uongozi katika eneo husika," amesema Dkt. Ndiege.

Mrajis ameyasema hayo katika Kikao cha siku mbili na Warajisi Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa, kilichofanyika Jijini Dodoma kuanzia tarehe 24 – 25 Machi, 2022 ambapo amewataka kushughulikia migogoro inayojitokeza kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na amesisitiza umuhimu wa kushirikiana na Wanasheria waliopo katika Ofisi za Mikoa katika kutatua migogoro inayojitokeza.

Baadhi ya Washiriki wa Kikao hicho cha Warajisi Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa na Menejimenti ya TCDC

Aidha, Mrajis wa Vyama vya Ushirika amewataka Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mikoa kuwa na Ushirikiano na Taasisi na Mamlaka nyingine zilizoko katika maeneo yao na kutoa ufafanuzi kuhusu Maendeleo na uendeshaji wa Ushirika ili kuwa na uelewa wa pamoja katika utekelezaji.

"Shirikianeni na kutoa taarifa za Utekelezaji na Mafanikio ya Sekta ya Ushirika kwa Taasisi na Mamlaka zilizoko katika maeneo yenu ili kufanikisha malengo ya Taifa katika kuimarisha Sekta ya Ushirika na kuinua Uchumi wa Wananchi kwa ujumla," amesema Dkt. Ndiege.

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAFUNZO KWA VYAMA VYA USHIRIKA KUIMARISHWA

Taasisi zinazohusika na maendeleo na usimamizi wa Sekta ya Ushirika nchini zimekubaliana kuimarisha Utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vyama Vya Ushirika wenye lengo la kuwajengea uwezo wanachama, viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika.

Taasisi zilizokutana leo Machi 23, 2022 Jijini Dodoma kwa lengo la kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Mpango huo ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Shirikisho la Vyama vya Ushirika nchini (TFC) na Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT).

Akizungumza katika kikao hicho, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, DKt. Benson Ndiege, amesema Kamati za Elimu na Mafunzo kwa Vyama vya Ushirika katika ngazi zote zinatakiwa kusimamia kikamilifu aina ya mafunzo yanayotolewa, wanaotoa mafunzo na wanufaika wa mafunzo hayo ili kupima ubora wake kwa Wanaushirika.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, DKt. Benson Ndiege, akizungumza kwenye kikao hicho.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Profesa Alfred Sife, amesema kuwa Chuo hicho kimeweka msisitizo kwa Taasisi ya Elimu Endelevu na Ofisi za Mikoa kufanya tathmini ya ubora wa mafunzo yanayotolewa kwa Wanaushirika ili mafunzo hayo yaendane na mahitaji ya jamii husika.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Profesa Alfred Sife, akizungumza kwenye kikao hicho

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Xavery Mkingule, amewataka watendaji kutoka katika Taasisi zinazohusika na maendeleo na usimamizi wa Sekta ya Ushirika nchini kushirikiana ili kuhakikisha kuwa Elimu ya Ushirika inayotolewa katika maeneo yao iwe inayokubalika na kuwanufaisha wanaushirika.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Xavery Mkingule, akizungumza kwenye kikao hicho.

Awali, akiwasilisha Utekelezaji wa Mpango huo wa mafunzo, Dkt. Gervas Machimu kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo ambaye ni Katibu wa Kamati ya Elimu na Mafunzo kwa Vyama vya Ushirika kitaifa amesema katika kipindi cha kuanzia Machi 2021 mpaka Februari 2022, Chuo kupitia ofisi za mikoa kimetoa mafunzo kwa wanachama, viongozi na watendaji 8,415 (wanaume 5,812 na wanawake 2,603) wa Vyama vya Ushirika nchini.

Dkt. Gervas Machimu kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi akizungumza kwaniaba ya Makamu Mkuu wa Chuo ambaye ni Katibu wa Kamati ya Elimu na Mafunzo kwa Vyama vya Ushirika kitaifa.

TCDC NA TANTRADE ZASAINI MKATABA WA MAKUBALIANO

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) wamesaini Mkataba wa Makubaliano kwa lengo la kuunganisha nguvu ya pamoja ili kutatua changamoto ya biashara hususan masoko inayowakumba wananchi ikiwemo wanaushirika ambao kwa kiasi kikubwa ni wakulima.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, DKt. Benson Ndiege (kushoto), na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Latifa M. Khamis wakisaini Mkataba wa Makubaliano. Wanasheria wa pande zote mbili wakishuhudia.

Makubaliano hayo yametiwa saini Machi 23, 2022 Jijini Dodoma na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, DKt. Benson Ndiege, na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Latifa M. Khamis.

Dkt. Ndiege amesema kutekelezwa kwa makubaliano haya kutaviwezesha Vyama vya Ushirika na Wanaushirika kuwa na uwezo wa kuzalisha kwa tija kulingana na mahitaji ya Soko, kutangaza bidhaa na mazao wanayozalisha na kufikia Masoko ya uhakika na endelevu.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, DKt. Benson Ndiege (kushoto), na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Bi. Latifa M. Khamis wakibadishana Mkataba wa Makubaliano.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, amesema ushirikiano kati ya TanTrade na TCDC utawanufaisha wakulima na Wanaushirika kupata masoko ya ndani na nje ya nchi kwa bidhaa wanazozalisha.

Makubuliano baina ya TCDC na TanTrade yanahusisha maeneo yafuatayo: Kutoa elimu na mafunzo ya kibiashara na masoko kwa viongozi, watendaji na wanachama wa ushirika; kuhamasisha makundi mbalimbali ya wananchi kuunda Vyama vya Ushirika; Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya kibiashara ndani na nje ya nchi; Kuratibu ziara na makongamano mbalimbali ya kibiashara kwa kushirikiana na vyama vya ushirika; Kuhamasisha na kuhimiza uwekezaji katika kuongeza thamani mazao na bidhaa za Tanzania; na Kubadilishana taarifa mbalimbali kuhusu uzalishaji, usafirishaji, masoko na takwimu za mauzo.

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YATEMBELEA SHAMBA LA USHIRIKA WA ZABIBU, CHABUMA AMCOS

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, tarehe 14 Machi, 2022 aliungana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji inayoongozwa na Mhe. Christine Ishengoma, ilioyotembelea Shamba la Zabibu la Ushirika wa Wakulima wa Chabuma AMCOS lililopo Wilayani Chamwino, Dodoma.

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, akiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji akiongea na Wakulima wa Shamba la Zabibu la Ushirika wa Wakulima wa Chabuma AMCOS.

Mhe Waziri Bashe amesema Serikali imedhamiria kuweka shamba hilo kuwa shamba la mfano la zao la Zabibu. Shamba hilo lenye Hekali 600 linamilikiwa na Chama cha Ushirika CHABUMA ambapo kupitia shamba hilo Serikali inalenga kupandisha thamani ya zao hili badala ya kuuza tunda pekee kuweka mashine zitakazochakata Zabibu na kutengeneza mchuzi ambao utauzwa kwa bei nzuri zaidi kuliko kuuza tunda pekee.

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, akiwa na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji Mhe. Christine Ishengoma ameshauri Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuweka Viongozi makini wa Vyama hivi vya Ushirika ili waweze kusimamia Ushirika wao kufikia malengo waliyojiwekea.

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, akiwa na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji .

KONA YA USHIRIKA WA KIFEDHA

USAJILI, UTOAJI WA LESENI NA USIMAMIZI

1:0 UTANGULIZI

Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), Miradi ya pamoja ya SACCOS, Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SCCULT) pamoja na Benki ya Ushirika zinasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2015. Aidha, Vyama hivyo mara baada ya kusajiliwa hutakiwa kuomba Leseni za uendeshaji wa biashara ya huduma za Fedha na husimamiwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Vyama vya ushirika, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha pamoja na Kanuni zake.

2:0 USAJILI NA UTOAJI WA LESENI KWA VYAMA VYA KIFEDHA

Hadi kufikia tarehe 31.03.2022, Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilikuwa na Jumla ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) vilivyokuwa vimesajiliwa ni 3,831, kati ya hivyo vilivykuwa pvimepewa Leseni ni 645 (SACCOS zenye Leseni daraja A ni 508 na zilizokuwa zimepewa Leseni daraja B ni 137).

3:0 USIMAMIZI WA SACCOS

SACCOS zimekuwa zikisimamiwa kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo Usimamia wa shughuli za chama nje ya ofisi zake (Off-site Supervision) na usimamizi chamani (On-site Supervision). Usimamizi nje ya chama hufanyika kwa njia ya kupokea taarifa za kila mwezi au robo Mwaka kutegemeana na aina ya Leseni iliyotolewa na Ofisi na tathimini hufanyika kwa kuzingatia viwango vya Kisheria (Prudential Standards) na viwango visivyo vya Kisheria (Non-Prudential Standards).
Mara baada ya kufanyika kwa tathimini hiyo, iwapo ofisi itabaini kuwepo kwa mapungufu kwenye taarifa zilizowasilishwa na Vyama husika, Ofisi huandaa utaratibu wa kwenda chamani kufanya ukaguzi (On-site Supervision) kwa lengo la kutathimini na kushughulikia mapungufu husika.

Hadi kufikia tarehe 31.03.2022 takwimu za kifedha kwa Vyama vya ushirika wa Kifedha (SACCOS) zilikuwa kama ifuatavyo;-

Mchanganuo wa SACCOS na umiliki wake	Mtaji	Jumla ya Mali	Jumla ya Akiba na Amana	Jumla ya Mikopo iliyotolewa
22 Largest SACCOS	41.99%	54.07%	58.59%	57.48
Other 623 SACCOS	58.01%	45.93%	41.41%	42.48%

Chanzo: Takwimu za TCDC 2022

Hali ya SACCOS imeendelea kuimarika kwa mujibu wa taathimini iliyofanywa na ofisi ya Mrajis kwa SACCOS zilizopewa Leseni hadi kufikia Machi 2022. Kwa mujibu wa tathimini hiyo, sehemu kubwa ya hali ya kifedha ya SACCOS inamilikiwa na SACCOS 22 pekee. SACCOS hizo 22 zinamiliki asilimia 41.99 ya mitaji yote iliyopo kwenye SACCOS, asilimia 54.07 ya Jumla ya mali zote, Asilimia 58.59 ya Jumla ya Akiba na Amana pamoja na 57.48 ya Mikopo yote iliyotolewa na SACCOS zenye Leseni nchini.

Aidha kwa lengo la kuendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za Vyama vya ushirika wa Kifedha, Kila SACCOS iliyopewa Leseni inapaswa kuhakikisha inatekeleza mambo yafuatayo;

i. Kuwasilisha taarifa za utendaji (Periodic Report) kila mwezi au robo Mwaka ifikapo au kabla ya siku saba mara baada ya kuisha kwa kipindi husika ili kuepuka adhabu zilizoweza kutozwa kwa SACCOS zitakazokiuka na kushindwa kuwasilisha taarifa husika.

ii. Kuhakikisha Bodi na menejimenti inawajibika kufanya Mikutano, Vikao, kuandaa nyaraka na kutekeleza matakwa ya Sheria, Kanuni na miongozo inayotolewa na ofisi ya Mrajis

iii. Kuandaa na kufunga hesabu kwa wakati na kuhakikisha Taarifa hizo zinakaguliwa kwa mujibu wa Sheria.

HITIMISHO;

Kila SACCOS inapaswa kuhakikisha inazingatia matakwa ya Sheria, Kanuni, Masharti, Miongozo na Sera za Vyama hivyo kwa lengo la kuongeza ufanisi, tija pamoja na ushirikishaji wa wanachama wao katika uendeshaji na utoaji wa huduma kwenye Vyama husika. Kila Kiongozi, mtendaji na mwanachama wa chama cha ushirika wa akiba na mikopo anapaswa kutekeleza wajibu wake chamani na kutathimini nafasi yake ili kufikia malengo ya uanzishwaji wa chama husika.

Aidha, kila Kiongozi na mtendaji wa SACCOS anapaswa kuweka mikakati thabiti na ubunifu utakaoendelea kuimarisha hali ya utendaji na utoaji wa huduma kwa wanachama wake. Jukumu la Serikali ni kuhakikisha maslahi ya wanachama yanalindwa na kuendelea kuwa salama ili kuwaongezea uwezo wa kushiriki kwenye shughuli za kuichumi na kijamii katika maeneo yao. Hivyo, Tume ya Maendeleo ya ushirika Tanzania kwa kushirikiana na mamalaka nyingine inaendelea kuandaa na kuweka mazingira wezeshi ya kuhakikisha SACCOS zinaendelea kuimarika na kufanya kazi zake vizuri na kwa kuzingatia matakwa ya Sheria nchini.

SACCOS YAIUNGA MKONO SERIKALI KATIKA UJENZI WA MADARASA MKOANI MBEYA

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha LULU SACCOS kimetoa mchanga na saruji kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, na madawati kwa shule za Jiji la Mbeya na pia kimetoa vyakula pamoja na mablanketi kwa magereza ya Jijini hapo.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, akipokea madawati kwa shule za Jiji la Mbeya kutoka kwa viongozi wa LULU SACCOS.

Msaada huo umetolewa wakati wa Maadhimisho ya Nane ya LULU SACCOS yaliyoanza tarehe 10 -12 Machi, 2022 Jijini Mbeya. Akikabidhi misaada hiyo yenye thamani ya Shilingi Milioni 15, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, kwa niaba ya LULU SACCOS kwa Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Laurian Patrick; amesema Msaada huo umetolewa kwa lengo la kutekeleza Msingi wa Saba wa Ushirika.

"Kati ya Vyama vinavyofanya vizuri LULU SACCOS ni mojawapo, naomba muendelee hivi hivi kwa haya mnayoyafanya ilimradi mnafuata Sheria, Miongozo Kanuni na Taratibu za Ushirika; tembeeni kwenye malengo yenu ili mfike mnapotaka kufika," amesema Dkt. Ndiege.

"Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan anapokuwa anasikia vitu kama hivi anaona kabisa Sekta ya Ushirika inamshika mkono katika juhudi zake za kuboresha elimu nchini," alisema Mrajis.
Awali, Mrajis wa Vyama ya Ushirika alitembelea Mafunzo ya Vyama vya Tumbaku kwa Mameneja Wahasibu na Maafisa Ugani yanayoendelea mkoani humo.

Dkt. Ndiege ameipongeza Kamati ya Elimu ya mkoa huo inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Mbeya, Richard Zengo, pamoja na waliojitokeza katika mafunzo hayo.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wanaushirika mkoani mbeya.

KONA YA USAJILI

MIONGOZO KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA

UTANGULIZI

Mrajis wa Vyama vya ushirika kwa mujibu wa Sheriaya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 amepewa dhamana ya kuandaa miongozo mbalimbali ya Vyama vya Ushirika ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya ushirika pamoja na Kanuni zake. Miongozo inalenga kutoa utaratibu wa namna ya utekelezaji wa majukumu ya Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya ushirika Na.6 ya Mwaka 2013, Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015, Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Misingi na Tunu za Ushirika, pamoja na Sheria nyingine za Nchi. Ufafanuzi huo unavirahisishia Vyama kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuondoa changamoto zilizopo hasa katika taratibu za ajira, fedha, uwekezaji, ukaguzi, ufilisi, manunuzi, utoaji wa elimu na mafunzo pamoja na taratibu za mawasiliano kwenye Vyama vya ushirika. Miongoni mwa miongozo iliyo andaliwa na kukamilika ni pamoja na:

I. Mwongozo wa Uandaaji wa kanuni za Uhasibu na Fedha kwa Vyama vya Ushirika

Mwongozo huu unatoa utaratibu kwenye Vyama vya Ushirika kuhusu namna bora ya kuandaa kanuni za uhasibu na fedha ambazo zitasaidia Vyama vya ushirika katika usimamizi wa masuala ya kifedha kwa ujumla.

Kanuni za uhasibu na fedha zinaainisha utaratibu wa namna shughuli za Chama zitakavyoendeshwa katika masuala yanayohusiana na matumizi ya rasilimali fedha pamoja na taratibu za kihasibu . Uwepo wa mwongozo huu utatoa picha halisi ya namna kanuni za uhasibu na fedha zinavyopaswa kuandaliwa na mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa katika uandaaji wa mwongozo huo.

II. Mwongozo wa Ufilisi

Mwongozo huu umelenga katika kufafanua taratibu za msingi za zoezi zima la Ufilisi wa Vyama vya Ushirika pindi vinapo futwa ili kuhakikisha kwamba wadau wote, hususan Maafisa Ushirika/ Warajisi Wasaidizi wanaelewa zoezi hili muhimu ili waweze kusaidia katika kuhakikisha kuwa linafanyika vizuri na kwa wakati.

Wafilisi wote wanaoteuliwa na Mrajis kufanya kazi ya ufilisi wa vyama vya Ushirika ni vema kuzingatia Mwongozo huu ili kuwarahisishia kutekeleza jukumu lao kwa ufanisi.

III. Mwongozo wa Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika wa Kifedha.

Mwongozo huu utakuwa ni nyenzo ya kumsaidia Afisa Ushirika Mkaguzi kufanya kazi ya ukaguzi kwa ufanisi, kuelekeza mambo muhimu ya kuzingatia na namna ya kutoa taarifa ya ukaguzi. Mkaguzi atapaswa kufanya uchambuzi wa shughuli za chama cha ushirika atakachokagua na kutoa taarifa.

Bodi ya chama itapaswa kuelimishwa juu ya hali halisi na mwenendo wa shughuli za uchumi za chama ikiwa ni pamoja na mbinu za kuboresha ufanisi wa shughuli za chama husika. Mwongozo huu unatoa mwelekeo wa ukaguzi wa vyama vyote vya ushirika vya Msingi, Miradi ya pamoja ya kiushirika, vyama vikuu vya ushirika na Shirikisho la Vyama vya Ushirika.

Pia mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kutoa utaratibu na maelekezo ya namna ya kufanya ukaguzi katika Vyama vya Ushirika nchini, na kufafanua masuala mbalimbali yanayopasa kuzingatiwa kabla na baada ya kufanya ukaguzi katika Chama cha Ushirika.

Kwa muktadha huu, Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini imetoa mwongozo huu, kwa Maafisa Ushirika wote nchini, pamoja na wadau wengine wa ushirika ambao kwa namna moja au nyingine watahusika na mwongozo huu, kufuata na kutekeleza utaratibu na maelekezo yote yaliyopo, kwa lengo la kuondoa changamoto zilizopo kwenye zoezi zima la ukaguzi katika Vyama vya Ushirika.

IV. Mwongozo wa Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika visivyo vya kifedha

Mwongozo huu unalenga kuwawezesha Maafisa Ushirikaka kufahamu taratibu mbalimbali za kuzingatia wakati wa ukaguzi kwenye Vyama vya ushirika wa kifedha. Utasaidia kubaini dosari mbalimbali ambazo kwa mujibu wa Sheria na taratibu za uendeshaji wa Vyama vya ushirika.

V. Mwongozo wa Ununuzi

Mwongozo wa Ununuzi kwa ajili ya Vyama vya Ushirika umelenga kuongeza utawala bora na matumizi thabiti ya fedha za Vyama na kuondoa/ kupunguza matumizi mabaya ya fedha. Utekelezaji wa vifungu vya mwongozo huu utakuwa na faida na manufaa kwa vyama vya ushirika kwani utaongeza umahiri na ufahamu wa shughuli za manunuzi. Hivyo basi, mwongozo huu utatumika kuimarisha ufanisi na uwezo wa Vyama katika kusimamia, kudhibiti na kutekeleza mchakato wa ununuzi.

Malengo makuu ya mwongozo huu ni kuhakikisha wajumbe wa bodi, watendaji na wasimamizi wa vyama vya ushirika wanakuwa na uelewa katika kufanya ununuzi na kuzingatia taratibu za ununuzi.

VI. Mwongozo wa uanzishwaji na uendeshaji wa mifuko ya maendeleo

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kuweka uelewa wa pamoja kwenye vyama vyote vya ushirika ambavyo tayari vimeshaanzisha mifuko na vile ambavyo vinatarajia kuanzisha mifuko kwa ajili ya kutekeleza shughuli.
Aidha vilevile utatoa maelekezo mahsusi kwa ajili ya Bodi za Vyama vya Ushirika kuhusu namna ya uanzishwaji na uendeshwaji wa mifuko ya maendeleo ndani ya chama, baada ya kuonekana kuwa baadhi ya vyama vimekuwa vikianzisha mifuko hii bila kuwa na utaratibu maalumu wa namna ya kuiendesha.

VII. Mwongozo wa Utatuzi wa Migogoro

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kuweka utaratibu utakaosaidia katika kutatua migogoro ya Vyama vya Ushirika kwa ufanisi kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika na Sheria nyingine za nchi.
Aidha, mwongozo umeanisha taratibu na ngazi za utatuzi wa Migogoro kutoka ngazi ya Chama chenyewe mpaka ngazi ya Rufaa. Aidha, utawezesha Vyama vyenyewe.

VIII. Mwongozo wa Udhibiti wa vihatarishi kwenye Vyama vya Ushirika wa kifedha

Mwongozo huu unalenga kuwezesha Vyama vya ushirika kuanda Sera zitakazoweza kuainisha vihatarishi ndani ya Chama cha Ushirika na kuweka njia mbalimbali za kuzuia au kuhepukana na vihatarishi hivyo ili Vyama vya ushirika visipate hasara ambazo zingeweza kuepukika.

IX. Mwongozo wa Uhamasishaji na Uanzishwaji wa Vyama vya ushirika

Kutokana na changamoto kubwa ya uhamasishaji na unzishaji wa Vyama vya Ushirika bila kufuata taratibu zilizoainishwa kwenye Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika imesababisha Vyama vinavyoanzishwa kutokuwa imara na endelevu. Hivyo ili kuhakikisha Vyama vinavyoanzishwa vinazingatia Sheria, Ofisi ya Mrajis imeandaa mwongozo huu ili kuwapatia wahamasishaji uelewa wa pamoja kuhusu namna nzuri ya uhamasishaji na uanzishaji wa Vyama vya ushirika.

MANUFAA YA KUANDAA MIONGOZO YA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA KUVISIMAMIA VYAMA VYA USHIRIKA NCHINI

Miongozo hii itarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Vyama vya ushirika kwa ufanisi mkubwa kwa kuwa itasaidia katika kutafsiri majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na kusimamiwa na vyama vya ushirika nchini. Mbali na kutafsiri utekelezaji wa majukumu itawezesha wasimamizi kuimarisha usimamizi kwa kusisitiza utekelezwaji wa Miongozo na kuhakikisha inafuatwa vyema na Vyama vyote vya ushirika.

Aidha, ni jukumu la kila Chama kuhakikisha kinapata nakala ya Miongozo kulingana na mahitaji kwa lengo la kuandaa Sera mbalimbali zitakazorahisisha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi na kwa kuzingatia Sheria.

WITO KWA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA UZINGATIWAJI WA MIONGOZO

Mrajis wa Vyama vya ushirika anatoa wito kwa vyama vya ushirika kuzingatia miongozo iliyotolewa katika kuandaa Sera mbalimbali zinazowezesha utekelezaji wa majukumu kwenye vyama vya Ushirika na kuhakikisha Sera hizo zinafuatwa na kuzingatiwa na Wanachama wote.
Vyama vya Ushirika vinapaswa kuahakikisha kuwa taratibu zote zinafuatwa katika uendeshaji wa Vyama vya ushirika. Taratibu hizo ni pamoja na ajira za watendaji kwenye Vyama vya ushirika,

KIKAO KAZI NA MAFUNZO KWA WATEKELEZAJI WA SHERIA YA USHIRIKA

Kikao kazi na Mafunzo kwa watekelezaji wa Sheria ya Ushirika kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa yote nchini kilifunguliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, Jijini Dodoma na kilifanyika kuanzia tarehe 9 - 11 Machi, 2022.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege (Katikati waliokaa) Akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wa TCDC na wanasheria kutoka ofisi za mikoa.

Kikao kazi hicho kiliandaliwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kilichofanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Conventional Centre na kiliwahusisha Wanasheria Kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa yote Nchini.

Mafunzo hayo yanahusu namna bora ya kutekelezaji Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 na Miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Ushirika ili kuwawezesha Wataalam hao wa Sheria kutoa Ushauri kwa Viongozi mbalimbali katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na Viongozi na Wanachama wa Vyama vya Ushirika.

Shani Mayosa, aliyekuwa Mkuu wa kitengo cha Sheria TCDC akishiki katika mkutano wa mafunzo ya wanasheria kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa Nchini.

Akizungumza katika ufunguzi wa Mafunzo hayo, Dkt. Ndiege amesema nafasi ya Wanasheria wa Mikoa katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Ushirika ni muhimu ili kuviwezesha vyama vya Ushirika viweze kupata ushauri wa karibu wa kisheria jinsi ya kutatua changamoto zinazojitokeza katika Uendeshaji wa Vyama; badala ya kusubiri Wanasheria wa TCDC kutoka Dodoma.

Baadhi ya wanasheria wakishiki katika kikao.

Mrajis amewaasa Wanasheria hao wa Mikoa kuvisaidia Vyama vya Ushirika katika kutatua migogoro mbalimbali inayojitokeza katika usimamizi na uendeshaji wa Vyama hivyo, na amewataka kutumia ipasavyo Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013, Kanuni na Miongozo ya Ushirika kwenye Ushauri watakaoutoa.

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI – 2022

TCDC YATOA MSAADA KWA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM WA KIJIJI CHA MATUMAINI, DODOMA

Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imetoa msaada wa chakula, mafuta, pempers na sukari kwa watoto wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi katika Kituo cha Matumaini Jijini Dodoma huku ukitolewa wito kwa Watanzania kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalumu.

KONA YA USIMAMIZI WA VYAMA VISIVYOKUWA VYA KIFEDHA

MKAKATI YA KUONDOA HATI MBAYA NA ZISIZORIDHISHA KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA VYA KOROSHO NA TUMBAKU

Sehemu ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika visivyo vya Kifedha imepanga kufanya usimamizi wa karibu Vyama vya Ushirika vinavyojihusisha na Mazao ya Korosho na Tumbaku. Katika hatua hiyo, Sehemu ya Ukaguzi na Usimamizi (IS) kupitia ofisi za Warajis Wasaidizi wa Mikoa pamoja na Maafisa Ushirika wa Wilaya imepanga kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo juu ya uandishi na utunzaji wa vitabu vya hesabu katika vyama vinavyojihusisha na Mazao husika.

Kutokana na ripoti ya ujumla ya hali ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika uliofanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya Vyama vya Ushirika 6,013 vilikaguliwa ambapo matokeo ya Ukaguzi yalikuwa kama ifuatavyo;

IDADI YA VYAMA VILIVYOKAGULIWA NA HATI ZILIZOTOLEWA KWA ASILIMIA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

AINA YA VYAMA	AINA ZA HATI ZILIZOTOLEWA																	
	HATI INAYORIDHISHA				HATI SHAKA				HATI ISIYORIDHISHA				HATI MBAYA				JUMLA	
MWAKA	2019/2020		2020/2021		2019/2020		2020/2021		2019/2020		2020/2021		2019/2020		2020/2021		2019/2020	
	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	%	IDADI	IDADI
SHIRIKISHO	0	0.00%	0	0.00%	1	0.02%	1	0.02%	0	0.00%	0	0.00%	0	0.00%	0	0.00%	1	1
UNION	0	0.00%	4	0.07%	19	0.32%	25	0.42%	12	0.20%	7	0.12%	11	0.18%	9	0.15%	42	45
AMCOS	34	0.56%	66	1.10%	1690	28.07%	1532	25.48%	605	10.05%	997	16.58%	1045	17.36%	1119	18.61%	3374	3714
SACCOS	223	3.77%	253	4.21%	1212	20.13%	928	15.43%	298	4.95%	228	3.79%	532	8.84%	470	17.82%	2269	1879
VINGINEVYO	28	0.47%	34	0.75%	192	3.19%	188	3.13%	33	0.55%	21	0.35%	82	1.36%	131	2.18%	335	374
JUMLA	**289**	**4.80%**	**357**	**5.94%**	**3114**	**51.72%**	**2674**	**44.47%**	**948**	**15.78%**	**1253**	**20.84%**	**1670**	**27.74%**	**1729**	**28.75%**	**6021**	**6013**

Kutokana na jedwali hilo, inaonekana kuwa matokeo ya ukaguzi kwa vyama vilivyokaguliwa kwa mwaka 2020/2021 yanaonesha kuwa jumla ya vyama 357 ambavyo ni sawa na asilimia 5.94% vimepata **Hati inayoridhisha,** Vyama 2,674 sawa na asilimia 44.47 % vimepata **Hati yenye shaka,** vyama 1,253 ambavyo ni sawa na asilimia 20.84% vimepata Hati isiyoridhisha na vyama 1,729 sawa na asilimia 27.74 vimepata **Hati mbaya.**

Kwa kuzingatia matokeo hayo, inaonesha kuwa Vyama vingi vimepata Hati zisizoridhisha na Hati mbaya jambo ambalo linatoa taswira mbaya kwa vyama na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kama wasimamizi wa vyama vya Ushirika nchini.

Kwa upande wa Vyama vya Ushirika visivyo vya Kifedha, hoja zilizojirudia katika vyama vingi ni kama ifuatavyo;

i. Udhaifu katika utunzaji wa taarifa za fedha katika vitabu;
ii. Udhibiti hafifu wa mikopo inayotolewa kwenye Vyama;
iii. Vyama kutokuandika miamala ya fedha kwenye vitabu kwa ukamilifu;
iv. Vyama kutokuwa na vitabu vya hesabu;
v. Kuwepo kwa udhaifu kwenye usimamizi wa mazao ya mkulima kutoka kwenya ghala la chama cha msingi kwenda ghala kuu; na
vi. Kutokutambulika kwa mali, madeni na hisa za Wanachama kwenye vitabu vya hesabu.

Kuna changamoto mbalimbali ambazo wakaguzi wamekuwa wakikutana nazo wakati wa ukaguzi wa Vyama vya Ushirika hususani Vyama vya Msingi vya Ushirika wa mazao. Changamoto kubwa zimekuwa ni watendaji wengi wa Vyama hivyo kutokuwa na vitabu vya hesabu kuanzia vitabu vya awali mpaka kitabu kikuu (leja kuu).

Pamoja na ukosefu wa vitabu hivyo, Wakaguzi wamebaini pia kwamba watendaji wa Vyama hivyo hawana ufahamu/Uelewa kuhusu vitabu hivyo pamoja na namna ya kuviandika vitabu vyenyewe.

Ili kupunguza au kuondoa kabisa hati mbaya na zisizoridhisha kwenye vyama vya Ushirika visivyo vya kifedha hususani vinavyojihusisha na mazao ya Korosho na Tumbaku kutokana na wingi wa vyama hivyo. Sehemu ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya ushirika visivyo vya kifedha kwa kushirikiana na COASCO wameandaa mfumo utakaosaidia kuweka uelewa wa kufanana kwa AMCOS zote zinazojihusisha na mazao ya Tumbaku na Korosho. Hii ni pamoja na utatekelezwa na kusimamiwa kwa karibu kupitia ofisi za Warajisi Wasaidizi wa Mikoa na Maafisa Ushirika utaondoa kwa kiasi kikubwa changamoto ya uwepo wa Hati mbaya na Hati zisizoridhisha kwenye Vyama vya ushirika.

Maandalizi ya vitabu vya mwongozo wa namna ya kuendesha zoezi hilo unaandaliwa na utakapokamilika matarajio ni kuwezesha wa utekelezwaji wa zoezi la kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kuhusu uandishi na utunzaji wa vitabu pamoja na namna ya kujibu hoja mbalimbali zinazotolewa na COASCO utaanza kufanyika kwa msimu huu wa 2022/2023.

SACCOS ZATAKIWA KUANDAA NA KUWASILISHA TAARIFA ZA UTENDAJI

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amevitaka Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), kuandaa na kuwasilisha taarifa za utendaji na uendeshaji kwa Wasimamizi ili waweze kufanya tathmini na kutoa maoni na ushauri kwa vyama husika. SACCOS zenye Leseni Daraja B zinatakiwa kuwasilisha taarifa kila Mwezi na SACCOS zenye Leseni Daraja A zinatakiwa kuwasilisha kila baada ya miezi mitatu.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege,(waliokaa wapili kushoto) akiwa na baadhi ya Washiriki wa Kikao Kazi cha Mameneja wa SACCOS na Wadau Kuhusu Usimamizi na Uendeshaji wa Shughuli za SACCOS zilizopewa Leseni.

Mrajis wa vyama vya Ushirika alikuwa akifungua Kikao Kazi cha Mameneja wa SACCOS na Wadau Kuhusu Usimamizi na Uendeshaji wa Shughuli za SACCOS zilizopewa Leseni, ambacho kilifanyika Jijini Dodoma kwa siku mbili kuanzia tarehe 8 Machi, 2022.

.

"Mnatakiwa kuhakikisha mnatumia muundo ulioandaliwa na TCDC badala ya kuwasilisha taarifa husika kwa kutumia muundo wenu usiozoendana na muundo uliotolewa na ofisi na kusababisha changamoto wakati wa kufanya tathmini," amesema Dkt. Ndiege.

Kila Mtendaji anayehusika kujaza na kuwasilisha taarifa hizo ametakiwa kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi na watakaoshindwa kuandaa na kutuma taarifa hizo kwa wakati, watatozwa faini ambazo watazilipa kutoka kwenye mshahara wake na si kutoka kwenye fedha za chama husika.

Dkt. Ndiege amezitaka SACCOS kupitisha na kuidhinisha bajeti yake kupitia Ofisi za Warajis Wasaidizi au Makao Makuu kutegemeana na ukubwa wa biashara husika, kufanya mikutano kwa mujibu wa Sheria, kushughulikia malalamiko ya wanachama kwa wakati pamoja na kuhakikisha zinatekeleza masharti ya Leseni za Vyama husika.

Washiriki wa Kikao Kazi cha Mameneja wa SACCOS na Wadau Kuhusu Usimamizi na Uendeshaji wa Shughuli za SACCOS zilizopewa Leseni.

SACCOS zimetakiwa kuhakikisha zinafanyia kazi Hoja za Ukaguzi wa Nje kwa lengo la kuondoa Hati Chafu. Amesema SACCOS zitakazoendelea kupata Hati Chafu, Watendaji wake (Meneja) watapaswa kuchukuliwa hatua ikiwemo kuondolewa kwenye nafasi yake kwa mujibu wa Kanuni ya 85(1)(g) ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha za Mwaka 2019 kutokana na kutokidhi sifa na vigezo vya kuendelea kuwa Meneja wa SACCOS.

Aidha, Mrajis amezitaka SACCOS kutumia Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi kwenye vyama. Amesema anafahamu kuna baadhi ya mifumo ina changamoto ya ufanisi kwenye utendaji lakini isiwe sababu ya kushindwa kutumia mifumo ya TEHAMA kwenye SACCOS.

"Iwapo patakuwa na tatizo lolote linalohusiana na watoa huduma wa Tehama ambao Ofisi yangu imewapatia vibali, mnapaswa kuniandikia barua ikielezea tatizo husika ili ofisi iweze kushughulikia na kuchukua hatua pale itakaposhindikana kutatuliwa kwa tatizo husika," amesema Dkt. Ndiege.
Mrajis amewataka Watoa huduma za TEHAMA katika Vyama vya Ushirika kuhakikisha wanaweka fomu zote 11 zilizoandaliwa na TCDC kwenye mfumo wao ndani ya mwezi mmoja kuanzia sasa ili kupunguza changamoto kwa SACCOS zenye mifumo kuandaa taarifa husika bila kutumia mifumo. Mifumo hiyo itaunganishwa (intergrated) na Mfumo wa Usimamizi wa TCDC unaoandaliwa.

SACCOS zimetakiwa kuendelea kubuni bidhaa na huduma ambazo zinaweza kuwavutia wananchi wengi kujiunga kwenye SACCOS na kuendana na mahitaji ya soko la fedha nchini. SACCOS nyingi zimekuwa zikiendelea kutoa huduma kwa mazoea na hivyo kushindwa kutafuta vyanzo mbadala vya fedha na kusababisha kuendelea kutoza riba kubwa na kwenda kinyume na lengo la kuanzishwa kwake.

WANAWAKE WALIOPO KATIKA SACCOS KANDA YA KASKAZINI WATOA VIFAA KINGA, HOSPITALI YA MAWENZI

Wanawake waliopo katika SACCOS Kanda ya Kaskazini (Manyara, Arusha, Tanga na Kilimanjaro) Machi 04, 2022 wametoa Vifaa Kinga katika hospitali ya Mawenzi iliyopo mjini Moshi. Shughuli hiyo imefanyika kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, 2022.

Vifaa vilivyokabidhiwa vitatumika katika wodi ya kinamama na watoto kwenye hospitali hiyo. Wanawake waliopo katika SACCOS Kanda ya Kaskazini wametoa vifaa hivyo ili kutekeleza Msingi wa saba wa Kuijali Jamii.

VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA VYA MAMCU NA TANECU VYATOA MILIONI 100 KUCHANGIA ELIMU, MTWARA

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amepokea Shilingi Milioni 100 kutoka Vyama Vikuu vya Ushirika vya MAMCU na TANECU kwa ajili ya kuboresha Elimu mkoani Mtwara.

Akipokea fedha hizo zilizotolewa na Vyama vya Ushirika, Brigedia Jenerali Gaguti amesema fedha hizo zitatumika kuhamasisha ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu na wanafunzi mkoani Mtwara.

"Fedha hizi zitumike kuchangia katika kuboresha Elimu na zisitumike kulipa posho kwa maofisa waliopo ofisini, ziwafikie walengwa; walimu na wanafunzi katika ngazi zote," amesema Mkuu wa Mkoa wa Mtwara.

BENKI YA USHIRIKA KILIMANJARO YAADHIMISHA MWAKA MMOJA KWA MAFANIKIO

Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL), Februari 03, 2022 imeadhimisha mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwake, ambapo Benki hiyo imefanikiwa pamoja na mambo mengine kutoa mikopo kwa Wakulima, Vijana, pamoja na Wafanyabiashara ndogondogo.

Maadhimisho hayo yamefanyika katika Manispaa ya Moshi, Mkoani Kilimanjaro ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, aliyewakilishwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Andrew Masawe.

Katibu Mkuu wa Wizara ya kilimo, Andrew Masawe, akizungumza katika Maadhimisho hayo.

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, katika hotuba iliyosomwa kwaniaba yake na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Andrew Masawe, ameitaka Benki ya KCBL kuendelea kutoa huduma za mikopo kwa Wakulima, Vijana, pamoja na Wafanyabiashara ndogondogo; na mikopo hiyo itolewe kwa riba nafuu.

Aidha, Benki ya CRDB imetakiwa kuendelea kuisimamia Benki hii ya Ushirika KCBL ili kuyatekeleza yote waliyoyapanga na kukubaliana.

Wadau mbalimbali walioshiriki katika Maadhimisho ya Mwaka Mmoja wa KCBL.

Waziri Bashe ameiagiza Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuendelea kuisimamia benki hii ya Ushirika ili iweze kufuata Misingi, Kanuni na Sheria za Ushirika katika uendeshaji wake.
Akizungumza katika Maadhimisho hayo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amesema TCDC itaendelea kusimamia Benki ya KCBL na kuendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika kununua Hisa katika Benki hiyo.

"Imetuchukua miaka miwili kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuhamasisha Vyama kulielewa wazo hili la kuwa na Benki ya Ushirika, haikuwa rahisi," alisema Mrajis.

VIONGOZI WA BODI YA TFC WALA KIAPO CHA MAADILI

Viongozi wapya wa Bodi ya TFC Januari 27, 2022 wamekula Kiapo cha Maadili kwa Viongozi mbele ya Mwanasheria wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania katika ofisi za Tume Makao Makuu Jijini Dodoma.

Viongozi wa Bodi mpya ya TFC wakila Kiapo cha Maadili ya Viongozi.

UJUMBE WA TANZANIA WAFANYA ZIARA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA NCHINI UGANDA

Ujumbe wa Tanzania umefanya ziara katika Vyama vya Ushirika nchini Uganda ambapo wametembelea pamoja na Vyama vingine Chama Kikuu cha Ushirika cha Ankole.

Chama cha Ankole kimeweza kumiliki kiwanda cha kuchakata Kahawa, pia kama Union huwa kinakopesha AMCOS hela kidogo za uendeshaji na badaye chama kinawanawakata wakiuza kahawa.

Ujumbe wa Tanzania wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Vyama vya Ushirika nchini Uganda.

Aidha, Union ya Ankole ipo kwenye mchakato wa kuanzisha SACCO ambayo itakuwa inafanya kazi ya kukopesha wanachama kama Taasisi inayojitegemea.

Chama kikuu cha Ankole walikuja kujifunza uendeshaji wa Ushirika Tanzania (KCU) mwaka 2010 na Sasa wamepiga hatua kubwa katika kushughulikia zao la Kahawa na uchakataji wake.

TANZANIA KUSHIRIKIANA NA BURUNDI KATIKA SEKTA YA USHIRIKA

Zabadilishana Uzoefu Kuhusu Usimamizi wa Vyama vya Ushirika

Ujumbe wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) umefanya ziara ya kikazi Nchini Burundi, na kufanya Kikao na wenyeji wao ambapo Mamlaka ya Uthibiti wa Vyama vya Ushirika Burundi (ANACOOP) waliwasilisha namna wanavyosimia Vyama vya Ushirika na TCDC iliwasilisha Majukumu yake, na baadaye kubadilishana uzoefu.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege (wapili kushoto) na ujumbe wake; wakiwa na Viongozi wa Ushirika Nchini Burundi.

Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege; na katika kikao hicho, Balozi wa Tanzania Nchini Burundi alihudhuria.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege akizungumza katika kikao cha pamoja na Viongozi wa Ushirika Nchini Burundi.

Aidha, ujumbe wa Tanzania ulitembelea Vyama vya Ushirika Nchini Burundi ili kujionea Mafanikio katika Sekta ya Ushirika.

Awali kabla ya ziara hiyo, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, tarehe 05/01/2022, alifanya Kikao kwa njia ya Mtandao na Balozi wa Tanzania nchini Burundi, Mheshimiwa Dkt. Jilly Maleko, kuhusu ushirikiano wa kiushirika kati ya Tanzania na Burundi. Hatua hiyo ni utekelezaji wa Maagizo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa alipofanya ziara nchini Burundi, Julai 16-17, 2021.

Akizungumza kwenye Kikao hicho, Dkt. Ndiege alisema katika ziara hiyo, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza Tanzania na Burundi kubadilishana uzoefu katika Sekta ya Kilimo na Mifugo hususan kwenye uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na kuongeza thamani ya mazao ya Kilimo.

"Ni matumaini yangu kupitia kikao hiki tutaweza kujadili vyema maeneo ya ushirikiano katika shughuli za vyama vyetu vya Ushirika na vyama vilivyopo nchini Burundi," alisema.

Dkt. Ndiege alisema Tume ipo tayari kuhamasisha Vyama vya Ushirika kwenda kubadilishana uzoefu wa Ushirika nchini Burundi na wao kuja kujifunza namna Ushirika unavyofanya kazi nchini Tanzania. Amebainisha kuwa Tume imekuwa ikifanya kazi ya kuviunganisha vyama hivyo na fursa mbalimbali zikiwepo za masoko na uwekezaji ndani na nje ya nchi.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika amesema kuna vyama vya ushirika 9,185 nchini ambapo kati ya hivyo 4,039 ni Vyama vya ushirika wa mazao.

Kwa upande wake, Balozi Maleko, alisema kumekuwapo na changamoto pale ubalozi unapohamasisha Watanzania kulitumia soko la mchele nchini Burundi kutokana na wanunuzi kuwa kwenye ushirika. Hivyo, changamoto hii inaweza kutatuliwa iwapo kutakuwa na Ushirikiano wa kiushirika kati ya nchi hizo mbili.

"Mtanzania akiingiza mchele Burundi anakutana na uongozi wa Chama cha Ushirika, na anaweza asiuze kwa faida kutokana na kukosa 'connection' nzuri, kwa kuwa wenzetu wana Ushirika kwenye mazao ya nafaka," alisema Mheshimiwa Balozi Maleko.

TUME YA USHIRIKA NA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI ZAANDAA MPANGO KAZI WA KUIMARISHA USHIRIKA KATIKA SEKTA YA MIFUGO

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Msajili wa Bodi ya Maziwa, Bodi ya Nyama pamoja na wadau wa maendeleo ya Ushirika ambao ni Heifer Program International walikutana Jijini Dodoma kwa lengo kuandaa Mpango Kazi wa Maendeleo ya Ushirika katika Sekta ya Mifugo.

Maandalizi ya Mpango huu yametokana na mkakati uliopo wa uhamasishaji na uanzishaji wa Vyama vya ushirika vya ufugaji 300 katika mikoa ya ufugaji Tanzania bara.
Uhamasishaji wa uanzishaji wa Vyama vya Ushirika vya ufugaji katika sekta ya mifugo umejikita katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025, Mpango Mkakati wa Tume 2021/2022 - 2025/2026 TMLP na ASDP II.
Taarifa zinaonyesha kuwepo Vyama vya Ushirika vya Mifugo 206 katika mikoa yote ya Tanzania Bara ambavyo vinatoa huduma kwa wanachama wake na jamii inayoizunguka kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini: -

NA	MKOA	IDADI
1	Arusha	9
2	Dar Es Salaam	10
3	Dodoma	3
4	Geita	10
5	Kagera	23
6	Katavi	1
7	Kigoma	1
8	Kilimanjaro	11
9	Manyara	5
10	Mara	21
11	Mbeya	50
12	Morogoro	5
13	Mwanza	1
14	Njombe	18
15	Pwani	4
16	Shinyanga	1
17	Tanga	21
18	Songwe	12
JUMLA YA VYAMA VYA USHIRIKA		**206**

Wajumbe wakijadili kwa pamoja maandalizi ya Mpango Kazi wa maendeleo ya Ushirika katika Sekta ya Mifugo

Katika kikao hicho maazimio yafuatayo yalifikiwa

I. Mpango Kazi utajikita katika kutoa elimu juu ya dhana ya ushirika kwa wafugaji kote nchini kwa lengo la kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Ushirika katika maeneo yao.
I. Uandaaji wa Mwongozo wa usimamizi thabiti wa Vyama vya ushirika katika sekta ya mifugo kufikia juni 2022.
II. Uandaaji wa Mwongozo wa ufanyaji biashara wa mazao yatokanayo na ufugaji kama vile maziwa, nyama na mazao mengine kutegemeana na uzalishaji kupitia Vyama vya Ushirika kufikia juni 2022.
III. Kuhuisha Vyama vya Ushirika vya ufugaji sinzia katika mikoa yote ya Tanzania bara ili viweze kutoa huduma kusudiwa kwa wafugaji na wanachama wa vyama hivyo.
IV. Kuvifikia vikundi vya ufugaji vinavyofanya shughuli za kiuchumi na vyenye mwelekeo wa kiushirika na kuvibadilisha kuwa Vyama vya Ushirika.
V. Kuwepo kwa hati ya Makubaliano kati ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Wizara ya Mifuko na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Bodi ya Maziwa Tanzania na Bodi ya Nyama Tanzania ili kuweza kurahisisha usimamizi wa sekta na bidhaa zake kufikia Juni 2022.

TCDC SACCOS YAANZISHA UWAKALA WA HUDUMA ZA KIFEDHA

CHAMA cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (TCDC SACCOS Limited), kimejipanga kuanzisha miradi mbalimbali ikiwamo uwakala wa huduma za kifedha kwa mitandao ya simu na benki ili kuongeza mapato ya chama na kujenga mtaji wa ndani. Mwenyekiti wa Chama hicho, Aron Ibrahim ameyasema hayo kwenye Mkutano Mkuu wa chama hicho uliofanyika jijini Dodoma.
Amesema wanachama kupitia Mkutano wameshauri Bodi ya Uongozi kuomba kibali kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika ili aruhusu kuendesha biashara ya uwakala wa mitandao ya simu pamoja na uwakala wa benki.

Wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (TCDC SACCOS Limited), wakiwa katika Mkutano Mkuu wa mwaka.

Vile vile, Mwenyekiti huyo amesema chama kitaendelea kuhamasisha Watumishi kujiunga na SACCOS hususan wa Mikoani na Wilayani, na kuendelea kufuatilia na kutoa hamasa kwa wanachama kumalizia kununua kiwango cha Hisa kinachohitajika na kuendelea kuweka Akiba kila mwezi.

Awali, akitoa taarifa ya ukaguzi, Mkaguzi kutoka Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), CPA Dora Meta, amesema kuwa Hesabu za chama zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, mwaka 2019 zimezingatia viwango vya Ukaguzi.

Mkaguzi kutoka Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), CPA Dora Meta, akiwasilisha Hesabu za TCDC SACCOS zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2019.

"Katika ukaguzi wa chama kwa mwaka 2019 chama hakikupata hoja yoyote kwa kuwa hoja zilizojitokeza kwa miaka miwili ya nyuma mwaka 2017 na mwaka 2018 ambapo ilikuwa hoja ya kutumia 'cash basis' badala ya 'accrual basis', kamati ya usimamizi kutotekeleza majukumu yake; hoja hizi zilifanyiwa kazi kipindi cha ukaguzi wa mwaka 2019. Tunaipongeza Bodi ya TCDC SACCOS kwa Usimamizi mzuri,"amesema CPA Dora Meta.

WAJUMBE WA BODI NJORECU WAPATIWA MAFUNZO YA UONGOZI NA UTAWALA BORA

Wajumbe wa Bodi Mpya ya Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Njombe (NJORECU), wamepatiwa Mafunzo ya kwa Siku mbili kuanzia Machi 29, 2022 kuhusu uendeshaji wa Vyama vya Ushirika.

Wajumbe wa Bodi Mpya ya Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Njombe (NJORECU), wakipatiwa Mafunzo.

Mafunzo hayo yaliyofanyika Mjini Njombe yalihusisha Uongozi na Utawala Bora katika Vyama vya Ushirika; ambapo Viongozi wa NJORECU wameweza kujaza fomu maalum ya "Tamko la Maslahi, Mali na Dhima kwa Kiongozi wa Chama" chini ya Kanuni ya 87 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015 na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

Mafunzo haya yametolewa na Ofisi ya Mrajis kupitia Mrajis Msaidizi Mkoa wa Njombe kwa ushirikiano na Mwanasheria kutoka Sekretariate ya Mkoa wa Njombe.

MAFANIKIO YA USHIRIKA SHINYANGA: AMCOS YANUNUA TREKTA

AMCOS ya Gimagi iliyopo wilayani Kishapu katika mkoa wa Shinyanga imenunua trekta lenye thamani ya Shilingi Milioni 41 kutoka kampuni ya Agricom Africa.

Zoezi la kukabidhi trekta aina ya Swalaj 855 kwa AMCOS ya Gimagi lilifanywa na kampuni ya Agricom Africa na kushuhudiwa na Mkuu wa wilaya ya Kishapu, viongozi wa AMCOS mbalimbali na watumishi wa Halmashauri ya Kishapu tarehe 21.03.2022.

Trekta aina ya Swalaj 855 lililokabidhiwa kwa AMCOS ya Gimagi.

Gimagi AMCOS kupitia ushuru wake uliopatikana kutokana na kukusanya na kuuza Choroko na Pamba msimu uliopita imefanikiwa kulipia trekta hilo tasilimu Shilingi 13.5 milioni na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imewapatia mkopo wa Shilingi 27.5 Milioni utakaolipwa kwa miaka 3 wenye riba ya asilimia 12.

Limetolewa na
Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)
Mtaa wa Kuu, S. L. P. 201, DODOMA.
Simu: +255 26 23 22456, Telefax: +255 26 23 21973
B.Pepe: ushirika@ushirika.go.tz Tovuti: www.ushirika.go.tz